


# Yesu Alijiita:

# “Mwana wa Adamu"

Hujambo!   Natumai umwema asubuhi ya leo.

Kuna wasomi ambao hawakubali Uungu wa Mwana wa Mungu, Yesu.

Wanamtangaza kuwa si zaidi ya mwanadamu; Kwamba Yesu ni nabii au labda ni  mwalimu mzuri wa maadili – hakika si mwili wa nafsi ya pili ya Mungu wa Utatu.

Kwa hiyo wanaelezaje imani ya Kikristo ya mapema kwamba utimilifu wa Mungu ulikaa ndani ya Yesu? – Kwa kudai kwamba wanafunzi walitumia ulaghai kufanya madai haya kuhusu Yesu ili kuendeleza harakati baada ya Yesu kufa na kuzikwa (wanadai hakuwahi kufufuka!).

**LAKINI YESU ALISEMAJE KUJIHUSU YEYE MWENYEWE?** Acheni tuchunguze jinsi Yesu alivyojitambulisha kwa majuma machache yaliyofuata.

Tutaanza wiki hii kwa jina la MWANA WA ADAMU (BINADAMU). Yesu alijiita “mwana wa binadamu” mara sitini na tano (65) hivi katika vitabu vya Injili. Kwa hiyo alimaanisha nini hapo? Ili kujibu swali hilo tunaona kwanza kwamba “mwana wa Adamu” ulikuwa msemo wenye mizizi ndani ya Agano la Kale.

**MWANA WA ADAMU KATIKA AGANO LA KALE;**

Katika Agano La Kale msemo wa “Mwana wa Adamu” una maana mbili tofauti sana.

- Kwanza unamaanisha “mtu” AMA  “binadamu”:

> **HESABU 23:19 a-** “*Mungu si mwanadamu, aseme uongo, wala si mwanadamu hata atubu;*”
>
> **ZABURI 144:3-** “*Ee BWANA, mtu ni kitu gani hata umjue? Na binadamu hata umwangalie?”*
>
> **Ezekieli 2:1-** [*Mungu akizungumza na Ezekieli*], “*Mwanadamu, simama kwa miguu yako, nami nitasema nawe.”*

- Lakini msemo  wa “Mwana wa Adamu” una maana ya pili ya Kiungu:

> **Danieli 7:13-** “*Nikaona katika njozi za usiku, na tazama, mmoja aliye mfano wa mwanadamu akaja pamoja na mawingu ya mbingu akamkaribia huyo mzee wa siku, wakamleta karibu naye.* [14] *Naye akapewa mamlaka, na utukufu, na ufalme, ili watu wa kabila zote, na taifa zote, na lugha zote, wamtumikie; mamlaka yake ni mamlaka ya milele, ambayo hayatapita kamwe, na ufalme wake ni ufalme usioweza kuangamizwa.*

Kwa hivyo katika msemo wa “Mwana wa Adamu” ambao Yesu alitumia mara nyingi kujirejelea, tunapata mchanganyiko wenye nguvu wa ubinadamu na Uungu.

Usiku ule ambao Yesu alikamatwa na kuhukumiwa, Kuhani Mkuu alimtaka ajitambulishe mwenyewe:

> **Mathayo 26:63-** *Lakini, Yesu akanyamaza. Kuhani Mkuu akamwambia, Nakuapisha kwa Mungu aliye hai, utuambie kama wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu*.” [64] “*Yesu akamwambia, Wewe umesema; lakini nawaambieni, Tangu sasa mtamwona Mwana wa Adamu ameketi mkono wa kuume wa nguvu, akija juu ya mawingu ya mbinguni..*”

Yesu alijitambulisha kwa uwazi kama ‘Mwana wa Adamu’ katika Danieli 7 na baraza la Mafarisayo na Masadukayo lilielewa wazi kwamba Yesu alikuwa akidai kuwa wa Mungu:

> **Mathayo 26:65-** *Ndipo Kuhani Mkuu akararua mavazi yake, akisema, Amekufuru; mna haja gani tena ya mashahidi? Tazameni, sasa mmesikia hiyo kufuru yake*. [66] *mwaonaje ninyi? Wakajibu, wakasema, Imempasa kuuawa’*.

**YESU ALITUMIA MSEMO WA "MWANA WA ADAMU" KWA NJIA TATU TOFAUTI:**

- MWANA WA ADAMU ALIKUJA DUNIANI KAMA MWANADAMU[1]

Alikula, akanywa, akalala, akafundisha, akahudumu, alisalitiwa, alihukumiwa kwa uongo, akafa na kufufuka.

- MWANA WA ADAMU ALIKUJA AKIWA MTUMISHI MWENYE MATESO[2]

Akitimiza ***Isaya 53:12*** Yesu alikufa msalabani ili kuchukua dhambi za ulimwengu.

- MWANA WA ADAMU ATATOKEA MWISHO WA NYAKATI ILI KUUDHIBITISHA UFALME WA MUNGU DUNIANI KWA MIAKA elfu moja (1000)[3]

**Mathayo 24:30** "*ndipo itakapoonekana ishara yake Mwana wa Adamu mbinguni; ndipo mataifa yote ya ulimwengu watakapoomboleza, nao watamwona Mwana wa Adamu akija juu ya mawingu ya mbinguni pamoja na nguvu na utukufu mwingi.*."

**MUHTASARI WA HAYA YOTE:** Kwa kutumia msemo wa "mwana wa Adamu" Yesu alidai ubinadamu wa Kimasihi na Uungu wa Kimasihi.

**MASWALI:**

- Je, huyu ndiye Yesu unayemjua?
- Je, huyu ndiye Yesu unayemwabudu?
- Je, huyu Yesu amekusamehe dhambi zako na kukupa uzima wa milele?
- Je, huyu ndiye Yesu unayeshiriki na wengine?

**WIKI IJAYO:** Yesu anaendelea kutuambia yeye ni nani.

Ubarikiwe sana katika jina la Yesu.
Ni wako-




Douglas Van Devender
Huduma za 'Jesus Ministries International' na 'Transforming Prayer'.

***maelezo ya chini:***

1 *ona*- Marko 2:10, 27; Mathayo 8:20; Mathayo 11:19; Mathayo 13:37; Mathayo 16:13; Luka 6:22; Luka 19:10; Luka 22:48

2 *ona*- Marko 8:31; Marko 9:9, 12, 31; Marko 10:33, 45; Marko 12:40; Marko 14:21, 41

3 *ona*- Marko 8:38; Marko 14:26, 62; Luka 12:40, Luka 17:24; Mathayo 13:41; Mathayo 16:28; Mathayo 19:28; Mathayo 24:30, 39; Mathayo 25:31; Luka 12:8; Luka 17:22, 30; Luka 18:8; Luka 21:36